## Minyoo fundo (Root knot nematode)

### Utangulizi

Minyoo fundo hupatikana kwenye maeneo ya hali ya hewa ya joto na baridi. Funza wa minyoo fundo uharibu mizizi ya migomba, hali hii huzuia usafirishaji wa maji na virutubisho muhimu vya migomba. Miche ya migomba iliyoshambuliwa na minyoo fundo hufa na migomba iliyozaa hutoa mazao pungufu.

### Dalili za uharibifu

Minyoo fundo hushambulia mizizi ya migomba na kusababisha fundo fundo kwenye mizizi kiasi ambacho mmea hushindwa kufyonza maji na virutubisho vya kutengeneza chakula cha mmea. Mimea iliyoshambuliwa na minyoo fundo ni kudumaa kwa mgomba na mizizi kuwa na ma-





### Udhibiti

- Zingatia usafi wa shamba wakati wote. kuruhusu mzunguko wa hewa shambani.
- Chonga mizizi na sehemu ya nje ya tunguu la mgomba kuondoa mizizi yote..



Udhibiti husishi wa bungua kwa kuzungushia vipande vya migomba kwenye mashina ya mgomba ili kuwavutia bungua wa migomba.




PIGA SIMU BURE:

**080 011 003 1**

P.O. Box 3024 , Arusha - Tanzania Nairobi Rd, Ngaramtoni Area

| Phone | Web | Email |
|---|---|---|
| +255 739 970 467 | www.tphpa.go.tz | dg@tphpa.go.tz |

tphpa_tz tphpa_tz TPHPA HABARI TV

SCAN FOR MORE


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA KILIMO

TPHPA TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES AUTHORITY

# MAMLAKA YA AFYA YA MIMEA NA VIUATILIFU TANZANIA

## WADUDU



# UDHIBITI HUSISHI WA VISUMBUFU VYA MIGOMBA

## Ugonjwa wa Mnyauko Fusari/Panama Mnyauko

**(Panama disease)**

### Utangulizi

Panama ni ugonjwa wa kuvu unaoathiri zao la migomba. Kuvu hawa huishi katika migomba iliyoambukizwa na kwenye udongo (hasa kwenye mashina yaliyooza) kwa hiyo ni rahisi kuambukiza migomba yenye afya kwa kutumia vitendea kazi

### Dalili za uharibifu

- Kubadilika kwa majani kuwa ya njano.
- Majani hubaki yamesimama kwa muda wa wiki mbili kabla ya kunyakuka na kuangukia kwenye shina la mgomba.
- Baadaye majani hugeuka kuwa na rangi ya kahawia nakukauka.
- Shina la mgomba lenye ugonjwa huonyesha madoa ya rangi ya zambarau na kahawia yanapokuwa yamekatwa.












### Udhibiti

- Panda miche bora ambayo haina maambukizi ya ugonjwa wa myauko fusari, ambayo inaw za kupatikana kwenye vituo vya utafiti kwa mfano; HORTI - Tengeru, ARI Mikocheni, Chuo kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA)..
- Ng'oa mashina ya migomba yaliyoathirika shambani yakauke yasisambaze ugonjwa.
- Panda miche yenye ukinzani kwa mfano; Wiliams, Pazi, Chinese Cavendish. Jamaica, FHIA17, FHIA 23 na Lacatan.
- Osha vitendea kazi vilivyotumika shambani kwa kutumia Jik (NaOCl)

## Ugonjwa wa Mnyauko Fusari/Panama Mnyauko

**(Banana Xanthomonas wilt). *Musacearum)***

### Utangulizi

Mnyauko huu husababishwa na Bakteria na unasambaa kutoka mgomba ulioathirika kwenda kwenye mgomba wenye afya kwa njia ya nyuki wasiouma na fumbu fumbu/Ua la kiume pamoja na vifaa vya kufanyia kazi, na kupanda miche iliyoathiriwa na ugonjwa. Ugonjwa huu usipodhibitiwa unaweza kuathiri uzalishwaji wa zao kwa asilimia 90.

### Dalili za uharibifu

- Ugonjwa huu hushambulia mgomba katik hatua zote za ukuaji
- Mnyauko unyanjano unasababisha majani machanga kuwa na rangi ya njano ambayo hugeuka kuwa kahawia hatimaye hunyauka.
- Baadaye majani hugeuka kuwa na rangi ya kahawia nakukauka.
- Kukauka kwa fumbufumbu, na matunda huiva wakati mkungu wa ndizi ukiwa mchanga.







### Udhibiti

- Zingatia usafi wa shamba na panda miche yenye afya,
- Panda miche yenye ukinzani kwa mfano; Wiliams, Pazi, Grand-Nine, Chinese Cavendish. Jamaica, FHIA 17, FHIA 23 na Lacatan.
- Tumia zana safi zilizochomwa moto au kutumia 'bleach' kukatia na kuondoa maua dume kupunguza maambukizi kupitia wadudu wanaobeba bakteria wanapofyonza nta yamaua
- Ng'oa migomba iliyoathirika na kuteketeza ili kuzuia kuenea kwa maambukizi
- Ondoa fumbufumbu kwa kutumia jiti lenye ncha mbili baada ya chane ya mwisho kutoka

## Ugonjwa wa Mnyauko Fusari/Panama Mnyauko

**(Black Sigatoka)**

### Utangulizi

Sigatoka nyeusi ya Migomba husababishwa na kuvu aina ya Mycosphaerella fijiensis. Ugonjwa huu husambazwa kwa upepo na mvua, majani hufa mara tu baada ya maambukizi, hali ambayo hupunguza mavuno ya ndizi kwa kiwango cha zaidi ya asilimia 50.

### Dalili za uharibifu

- Mistari midogo ya majano au myeusi au madoa huonekana chini na juu ya jani, na baadaye hugeuka kuwa kijivu hatimaye hukauka.
- Husababisha matunda ya ndizi kuiva kabla ya kukomaa.







### Udhibiti

- Ondoa majani yaliyoathirika, choma kumia kusambaa kwaugonjwa
- Usipande migomba kwenye maeneo yenye kutuamisha maji.
- Punguza majani ya migomba na miche kuruhusu mzunguko wa hewa ya kutosha shambani
- Panda miche yenye ukinzani kwa mfano; Williams, Pazi, Grand-Nine, Chinese Cavendish, Jamaica, FHIA 17, FHIA 23, na Lacatan.